## *HABARI FUPI*



### Mashemasi wamekuwa Mapadri

Mashemasi Giovanni, Marko, Riccardo na Gianpiero, waliohudumia Ol Moran miezi iliyopita, walipadrishwa kule Venisi Jumamosi 22 Juni. Tuendelee kuwaombea tukiwakumbuka kwa shukrani na upendo.

### Harambee ya Kwaya

Wanakwaya wa Parokia wtakuwa na Harambee Jumapili 18 Agosti, Ol Moran. Lengo lao ni kununua vyombo vya muziki na pia kusimamia mashindano na kazi zao nyingine. Hivyo, wanaendelea na mazoezi ya nyimbo kufuatana na mpango wa "Singing Together".



### Vyama

Kina Mama wa Parokia walikutana Ngare Narok kwa siku ya Michezo iliyopangwa na chama cha CWA, Jumamosi 22 Juni. Hata vyama vingine vya CMA na CA vinaendelea na mipango na mikutano ya mwaka huu.



### Mashindano ya PMC

Watoto wa PMC wameanza Mashindano ya Mwaka Huu, Jumamosi 21 Julai, kati ya Makanisa yetu. Washindaji wataendelea na Mashindano ya Jimbo, Jumamosi 24 Agosti kule Igwamiti.

### Vijana



Vijana walifanya Uchaguzi mwezi wa sita na Viongozi wapya waliianza masomo ya Uongozi yatakayoendelea hata Agosti kwenye Zones. Miezi hii Vijana wanaendelea na shughuli zao kwenye Makanisa Madogo.

### Makatekista

Makatekista walikuwa na siku ya maombi na mkutano Ijumaa 9 na Jumamosi 10 Agosti. Siku hizo walifanya uchaguzi wa Kamati ya Makatekista na Waakilishi wao katika Halmashauri Kuu.

Kuna pia mabadiliko ya uteuzi: bw. John Wanyama aliteuliwa kwa Makanisa ya Nagum na Dam Mbili; bw. Jacob Ngetich kwa Kanisa la Ndunyuriwo; bw. James Thuo kwa Kanisa la Miharati. Mabadiliko mengine yatafanyika baada ya kumalizia Uchaguzi wa Parokia.

### Shirika la Masista

Nyumba ya Masista imeona mabadiliko kadhaa. Sr. Veronika aliyekuwa anafanya kazi kwenye Dispensary, alitumwa Italia. Sr. Agnes alitumwa Philippines. Hapa Ol Moran amerudi Sr. Mary, atakayeshikilia kazi ya nyumba ya Watoto "The Magnificat". Pia wametumwa Ol Moran Sr. Gerusa na Sr. Mamisoa.

### Saint Martin yatimiza miaka 20

Shirika la Saint Martin Catholic Social Apostolate latimiza miaka 20 tangu mwanzo wake mwaka 2009. Kutakuwa na Sherehe Jumamosi 9 Novemba kule Nyahururu: wamealikwa wanaofanya kazi na St. Martin, pia wanaosaidiwa nao, na Wakristu wote.

Hata katika maeneo mbalimbali ya Jimbo kutakuwa na nafasi ya kukumbuka kazi za miaka hiyo yote na kushukuru wanaojitolea katika huduma hiyo: hapa kanisani Ol Moran itakuwa Jumapili 18 Agosti.

**Kalenda ya Agosti 2019**

**MAIN ACTIVITIES AND SUNDAY GOSPELS**

*Alhamisi 15 Agosti* - ***Sherehe ya Maria Kupalizwa Mbinguni***
→ 07.00am: Ol Moran, Misa ya Sherehe

*Jumamosi 17 Agosti*
→ 10.00am: Kahuho, Sherehe ya Vijana

*Jumapili 18 Agosti* - ya 20 ya Mwaka *(Lk 12:49-53)*
→ Misa - 7am: Survey; 9am: Miharati, Ngare-Narok; 11am: Nagum
→ Ol Moran, 11am: Misa na Sherehe ya Saint Martin; Harambee ya Kwaya (baada ya Misa)

*Jumamosi 24 Agosti*
→ 09.00am: Igwamiti, Mashindano ya PMC ya Jimbo la Nyahururu
→ 10.00am: Ol Moran, Sherehe ya Vijana

*Jumapili 25 Agosti* - ya 21 ya Mwaka *(Lk 13:22-30)*
→ Misa - 7am: Kabati; 8am: Gituamba; 9am: Githima; 10am: Posta; 11am: Ol Moran

*Jumapili 1 Septemba* - ya 22 ya Mwaka *(Lk 14:1.7-14)*
→ Misa - 9am: Magadi, Lounyek; 10.30am: Dam Mbili; 11am: Ol Moran; 12noon: Ndunyuriwo

*Jumamosi 7 Septemba*
→ Ngare Narok, 10am: Parish Education Day (Tumaini na Hekima), na uzinduzi wa mradi wa Kijito

*Jumapili 8 Septemba* - ya 23 ya Mwaka *(Lk 14:25-33)*
→ Misa - 7am: Ol Motunyi; 8am: Minjore; 9am: Kahuho; 10am: Mithuri; 11am: Ol Moran; 12noon: Mbombo

*Jumamosi 14 Septemba*
→ Ol Kalou, 10am: Harambee ya Jimbo kwa ajili ya Kirima Primary

*Jumapili 15 Septemba* - ya 24 ya Mwaka *(Lk 15:1-32)*
→ Misa - 7am: Survey; 9am: Miharati, Ngare-Narok; 11am: Nagum, Ol Moran

SAUTI *ya Mtakatifu* MARKO
*- No. 77, Year 11, Printed on 12th August 2019 - (NOT FOR SALE)*
**SAINT MARK** CATHOLIC PARISH - Ol Moran - *Catholic Diocese of Nyahururu*
*P.O.Box 20 - 20320 Kinamba - saintmark@olmoran.it - +254 720 924 153*
Printed by POP-SIGNS MEDIA
Nairobi - Tel. 0720 845 699 and 0724 236 271

**Mt. Marko Mwinjili na Msimamizi wa Parokia**
*Aliishi Yerusalemu. Baada ya ubatizo wake, akafuatana na Mtume Paulo. Kisha aliishi Roma na Mt. Petro, akaandika Injili akikusanya mafundisho yake. Akaeneza Ukristu na kuanzisha Kanisa Aleksandria ya Misri. Akawa Mhubiri, Askofu na Shahidi wa kwanza kwenye bara la Afrika.*

**Gazeti la Parokia Katoliki ya Mtakatifu Marko Mwinjili ya Ol Moran**
*N. 77 — Mwaka wa 11*
**Julai-Agosti 2019**

# SAUTI *ya Mtakatifu* MARKO

*Uchaguzi wa Kiparokia 2019*

# Kwa Mfano wa Kristu Mchungaji

Tunataka Viongozi wa aina gani? Swali hili ni muhimu kila wakati tunapofanya uchaguzi, hata tunapowatafuta Viongozi wa Kanisa.

Mwaka huu, kwenye Parokia yetu, ni wakati wa Uchaguzi, baada ya muhula wa miaka mitatu iliyopita. Katika Makanisa Madogo zimeshachaguliwa Kamati za Kanisa. Sasa tunaendelea kuwachagua Viongozi wa Jumuiya Ndogo Ndogo. Kisha tutatafuta Viongozi wa Zones na wanachama wa Halmashauri Kuu.

Katika masomo yanayofanywa kabla ya Uchaguzi, tumetazama mfano wa Yesu Mchugaji Mwema, ili kutafakari kuhusu aina ya Viongozi tunaohitaji.

Yesu alitumia mfano wa Mchungaji Mwema wakati alipoongea kuhusu uhusiano wake na wafuasi. "Mimi ni Mchungaji yule mwema, nanyi ni kondoo wa kundi langu" Yesu alisema.

Akisema hivyo, alitaja mema ya Mchungaji: yeye anawajali kondoo wake, huwajua na kuwaita kwa jina, yeye huwalinda, hadi kutoa nafsi yake kwa ajili ya kondoo. Nao kondoo wanajua sauti ya Mchungaji, na kumfuata.

> Viongozi wa Kanisa huitwa Wachungaji. Roho wa Kristu Mchungaji Mwema iwasaidie.

Jinsi ulivyo mzuri mfano huu! Ni mfano unaosema wazi kuhusu uongozi bora wa Kanisa. Ndiyo sababu katika Kanisa, Viongozi wenyewe huitwa Wachungaji: Maaskofu, Mapadri, kama vile Makatekista na Viongozi wa Makanisa wamepewa mfano huu kwa kufahamu majukumu yao.

Kwa mfano wa Yesu Mchungaji, Viongozi wa Kanisa wanatarajiwa kuwajua kondoo wao, kuwajali na kuwaongoza katika malisho mazuri, kujitolea kwa ajili yao na kuwalinda.

Hivyo nawatakia Viongozi waliochaguliwa kwa muhula huu mpya: roho ya Kristu Mchungaji iwasaidie katika majukumu ya kuwahudumia Wakristu na Kanisa.

Nawashukuru kwa kukubali wajibu huo. Mbarikiwe sana!

Fr. Giacomo Basso - *Baba Paroko*

*Mfano wa Yesu Mchungaji anayeongoza kundi lake*



## JIMBO LA NYAHURURU

HARAMBEE YA SHULE YA JIMBO → *Jimbo la Nyahururu litakuwa na siku ya kuchangia mradi wa ujenzi wa Shule ya Msingi ya Jimbo, itakayoitwa "Kirima Primary School", kwa kumbukumbu ya Askofu Mkuu Marehemu Kirima. Itajengwa kule Ol Kalou. Harambee itafanywa Jumamosi 14 Septemba 2019. Lengo ni kupata milioni 25 mwaka huu. Kila Parokia inatoa kiwango fulani, nasi pia tunaendelea kuchangia katika Makanisa, pamoja na mchango wa Jimbo wa kila mwaka.*

NATIONAL PRAYER DAY → *Siku ya Maombi ya Kitaifa itakuwa Jumamosi 5 Oktoba 2019, kule Subukia, kuanzia saa nne. Ibada hiyo hupangwa kila mwaka na KCCB (Kenya Conference of Catholic Bishops), kwa ajili ya majimbo yote ya taifa. Mada ya mwaka huu ni ile ya Mwaka wa Uenezaji wa Injili, yaani "Tumebatizwa na tumetumwa" (Baptized and Sent).*

MCHANGO WA NYUMBA YA WATOTO → *Jumamosi 15 Juni kulikuwa na Harambee nyingine kwa Jimbo, kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba ya Watoto (Diocesan Children's Center), itakayojengwa kule Equator, Nyahururu.*

Malkia wa Amani

## SHEREHE YA MARIA KUPALIZWA MBINGUNI

*Mwezi wa nane, tarehe 15, kuna Sherehe kubwa inayopendwa sana na Wakristu, tukiadhimisha Maria alipopalizwa mbinguni (Assumption of Mary). Katika Kanisa la Parokia, ni siku ya kumheshimu Maria mbele ya sanamu ya Malkia wa Amani.*

*Wakristu hujiweka kwa imani chini ya ulinzi wake na kujikabidhi kwa maombezi yake, ili tuishi na amani katika eneo letu na duniani kote, pia tuwe salama katika kumfuata Bwana wetu Yesu Kristu, tuweze kufika sisi wenyewe mbinguni kwake.*



*Sherehe ya Msimamizi na Mchango wa Jimbo*

## Matokeo ya Parish Baraka Day

*Ol Moran, Jumapili 12 Mei - Siku ya Parish Baraka Day, ikawa siku ya pekee, tulipomsherehekea Msimamizi Mtakatifu Marko Mwinjili na kumbukumbu ya kutabarukiwa Kanisa la Parokia. Ile siku CMA na CWA walifanya upya Nadhiri zao. Ikawa pia nafasi nzuri ya kusaidiana katika jukumu letu la kiparokia la kutimiza Mchango wa Jimbo la Nyahururu (Diocesan Budget): sadaka zote za shukrani kwa sababu ya baraka ya familia zilitolewa kwa ajili ya Jimbo (Kwa jumla KSh 154,100).*



*Juu:* Fr. John alipokata keki ya Sherehe ya Miaka Hamsini ya Upadrisho, hapa Ol Moran
*Kulia:* Fr. John pamoja na Viongozi na Mapadri wengine wageni

*Miaka 50 ya Upadrisho*

## Sherehe ya Fr. John



Padri Giovanni Volpato alikuja kututembelea mwanzo wa mwezi wa sita. Tulipata nafasi nzuri ya kusherehekea miaka hamsini ya Upadrisho wake, akihudumia Kenya kwa miaka 25, na Ol Moran kwa miaka 12, alipoanzisha Parokia yetu. Alikuja pamoja na Mapadri wengine watatu kutoka Venisi, kama vile Fr. Mario, Fr. Lucio na Fr. Francesco. Aliongoza Misa ya sherehe Jumapili 2 Juni. Hizo siku zingine alipata nafasi ya kutembelea makanisa na jumuiya kadhaa. Wakristu walimpokea kwa furaha na upendo, kama kila wakati. Karibu tena Fr. John!




Waseminarista Lawrence na John, pamoja na Fr. PK na Masista

### Waseminarista

Tumefurahia Parokiani huduma na kazi za Waseminarista waliokuwapo likizoni miezi iliyopita. Mseminarista Lawrence, kutoka Mithuri, alikaa Parokiani kwa muda wa miezi miwili. Baadaye, alitumwa kwetu hata Mseminarista John Edong'a, kutoka Marmanet, kwa muda wa majuma mawili. Mwishoni mwa Julai wakarudi kwenye Seminari kuendelea na masomo yao.

## Huduma ya Kiroho kwa Wagonjwa

Wagonjwa na wakongwe wa Parokia wanaendelea kutembelewa na Padri Peter nyumbani mwao, wakiletewa msaada wa Sakramenti na wa Sala ya Kanisa. Mpango bado unaendelea, na Makanisa yaliyobaki wakati huu ni Mbombo na Ol Moran. Viongozi wa Makanisa hutengeneza orodha ya wagonjwa, na kumsindikiza Padri kwenye ziara yake. Wakristu wa Jumuiya Ndogo Ndogo wamealikwa kuwa karibu wakati Padri anapowatembelea wakongwe, ili hawa ndugu na dada zetu waweze kuona ushirikiano wa Kanisa lote.



*Kulia juu:* Fr. PK akiwa kwa wagonjwa
*Kulia chini:* Baraka ya Kiekaristi kwa makutano ya barabara



### Baraka ya Kiekaristi

Hata mwaka huu tumerudia ibada takatifu ya Sakramenti ya Mwili na Damu ya Kristu, pamoja na Maandamano na Baraka ya Kiekaristi kwa ajili ya Parokia nzima, maboma, mashamba na mifugo. Ilifanyika Jumapili 23 Juni. Ibada hiyo ilifunga sherehe zinazofuata Sherehe Kuu ya Pasaka.





*Education Day: Hekima na Tumaini*

## Kijito Kipya Shuleni

TUMAINI ACADEMY - Maendeleo yameonekana Ngare Narok. Shule ya Parokia iko karibu kukamilisha kijito. Mradi huu umefadhiliwa na Shirika la Maisha Marefu (Milan, Italia). Umejengwa na Kampuni ya Pumpzen (Nanyuki) pamoja na bw. Peter Nyamu (Sipili). Maji yameshatoka na kutumika. Jumamosi 7 Septemba kutakuwa na Sherehe ya Elimu, Tumaini na Hekima pamoja (*Parish Education Day*), na kufungua mradi huo.

Walimu wa Tumaini walikuwa na safari yao, 23 na 24 Juni, kumtembelea mwalimu Brutha Peter Tabichi, aliyepata *Global Teacher Prize 2019*. Waliweza kuona miradi ya shule ya Kiriko (Nakuru) anapofanya kazi, na kupata mawaidha kwa kazi ya elimu. Tena, Wanafunzi wa madarasa wa 6-8 walikuwa na safari ya elimu Jumatano 31 Julai, kwenda Nakuru National Park.

HEKIMA HOUSE - Wanafunzi wa Hekima pia wamefunga muhula wa pili baada ya safari yao, tarehe 2 na 3 Agosti. Walitembelea Nanyuki kwenye Chumba cha Bunge ya Laikipia County, pia kwenye shule na sehemu nyingine.



*Juu:* Tumaini wakitembelea Nakuru National Park
*Chini:* Hekima kwenye Laikipia County Assembly Hall





*Tunpanda miti mingi, ijapokuwa makaa huendelea!*

## Mazingira ya eneo letu

*Mvua nzuri imerudi, mimea na mifugo imepata nguvu tena. Na Parokia imepata nafasi ya kuanzia tena mpango wa kupanda miti mingi kwenye Agroforestry na pia katika mashamba mengine. Mpango utaendelea hadi mvua itakapoturuhusu. Maskauti wa Mwamba wameshaanza kazi hiyo, vile vile wanafunzi wa Tumaini. Hata hivyo, ni huzuni kuona kwamba kazi ya kuchoma na kubeba makaa haramu zinaendelea katika sehemu mbalimbali za eneo letu, inayosababisha uharibifu wa mazingira, na hasara kubwa kwa wenyeji. Kwa mfano, Maskauti walitembea Jumamosi 21 Julai kwenye bonde la Ngoisusu, na bado walikuta majivu na moshi ya makaa yanayoharibu miti ya kitambo. Je, viongozi wa eneo wamefunga macho?*

*Maskauti wa Parokia wameendelea pia na kazi mbalimbali. Rovers walitembea Mithuri mwezi uliopita, tena mwezi huu wamesaidia kufyeka uwanja wa Parokia na kupata kuni. Mwamba walifanya Camp Mochongoi mwezi wa sita, kupanda miti na kuitafutia kuni Shule ya Upili ya Ol Moran.*



*Kushoto:* Maskauti wakipanda miti Gathanji
*Chini:* Scout Hike bondeni Ngoisusu





### Maendeleo ya Makanisa

Kuna miradi inayoendelea katika Makanisa Madogo kadhaa. Githima ujenzi wa kanisa jipya umesonga sana, hadi kufikia mabati. Tena, Kahuho Jumapili 14 Julai walibariki na kulilaza jiwe la kwanza la msingi wa mjengo wa kanisa la mawe.

Kule Mithuri wamekamilisha kazi ya vioo vipya, na kazi hiyo ilianzishwa hata Ol Moran, kando ya Kanisa Kuu. Miradi mingine katika Makanisa itaendelea hasa baada ya uchaguzi.

*Juu:* Jiwe la Kwanza la Kanisa la Kahuho
*Chini:* Maendeleo ya ujenzi wa Kanisa la Githima

